# Visasi na Risasi

Philipo Oyaro

©Philipo Oyaro 2020
Chapa ya kwanza 2020
Chapa ya pili 2022
ISBN: 978-9987-9759-2-1
SIMU: +255743499439
Baruapepe: philipo.oyaro@gmail.com

Kimechapishwa na:

PANGONI Publishers

S.L.P 41062
Dar es Salaam

SIMU: +255714839430/+255767839430

Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kuchapisha, kunakili au kukifanyia maigizo kitabu hiki pasipo ruhusa ya mwandishi. Hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka agizo hili.

Riwaya hii ni ya kubuni, na hivyo baadhi ya maeneo na majengo yaliyohusishwa hayana uhusiano na visa vilivyomo. Halikadhalika majina yaliyomo humu ni ya kubuni na huenda yakafanana na majina ya baadhi ya watu wanaoishi au waliofariki. Mwandishi anaomba radhi kwa usumbufu wote utakaojitokeza.

SHUKRANI
Shukrani zangu za dhati ziwaendee wote waliowezesha kukamilika kwa riwaya hii. Kwanza, Jeremiah Machira na kwa kuisoma na kutoa ushauri kuifanya iwe ya kuvutia zaidi. Pili, Mwalimu Wisahi Matiku na mwandishi John Wisse kwa uhariri. Tatu, wote waliotoa mchango wao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha uandishi na uchapaji wa riwaya hii.

# 1

Simu ya Noela Kuzi iliingiza ujumbe mfupi: *Nimekutumia kwa WhatsApp.* Alikuwa mwenye shauku kuu na mwenye nguvu licha ya siku ndefu ya uwezeshaji katika mafunzo. Aliwasha data kwa pupa; vidole vikikosea. Simu ilizizima pale ujumbe toka mitandao ya kijamii ulipoingia.

Aliingia WhatsApp na kubofya ujumbe toka kwa Julius. Kwa takribani dakika nne alisoma kilichokuwa kimeandikwa. Uso wake ulijawa na mshangao, mapigo ya moyo yakamwenda mbio. *Haya yote Julius ameyapata wapi? Je yana ukweli?* Alijikuta akiona haya kutilia shaka jambo lililowasilishwa na mume wake.

Aliharakisha na kuuacha ukumbi wa mafunzo. Nje kulikuwa na teksi iliyokuwa ikimsubiri. Aliketi kiti cha nyuma, "Nipeleke nyumbani," alimwambia dereva wa teksi hiyo aliyekuwa anapafahamu nyumbani kwao. Ubongo wake ulizama katika tafakuri mara tu baada ya teksi kuanza mwendo. Alitafakari juu ya Julius na harakati zake. Majuma kadhaa yaliyopita alikuwa amemweleza azma yake ya kuweka hadharani kashfa aliyodai kuwa inafumbiwa macho. Hakuwa ameafikiana naye na hivyo kumshauri kuziacha mamlaka husika zifanye kazi hiyo kwani ingeweza kuwa mwanzo wa kujenga chuki, visasi na pengine mauti. Jibu la Julius lilikuwa fupi: "Mamlaka husika zimelala usingizi

ngoja nipaze sauti huenda wakazinduka.”

Hakuwahi kupata dondoo mahususi za hoja za Julius na walengwa hadi alipokuwa akisoma hiki alichotumiwa kupitia mtandao wa kijamii. Kulikuwa na jina moja tu lililotajwa lakini kwa uzito wa kashfa yenyewe lazima wahusika walikuwa wengi na watu wazito katika medani ya siasa na utawala.

Muda anafika nyumbani baba yake alikuwa sebuleni. Alimsabahi na kuketi kwenye kochi. Ilikuwa ni bahati kwamba mafunzo hayo yaliyomtoa Dar es Salaam hadi Shinyanga yalimkutanisha na baba yake, Simon Kuzi, kapteni mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na mama yake, Suzan. Alikuwa amechagua kuishi nyumbani badala ya hotelini kwa muda wote wa mafunzo.

Noela alikuwa mtoto wa tatu katika familia hii ya watoto wanne. Dada yao mkubwa aitwaye Anna alikuwa ameweka nadhiri ya utawa akifuatiwa na, daktari Joel wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; na kisha Mdogo wao wa mwisho, Kuzi Jr. aliyefuata nyayo za baba yake na kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Hakwenda chumbani kama ilivyokuwa kawaida kwa siku hizi chache alizokuwa kwao atokapo mafunzoni, bali sebuleni kwenye kochi. Wakati huu hakutaka kusoma taarifa ile kupitia simu. Udogo wa kioo cha simu ulimnyima uhondo hivyo akaifungua kompyuta mpakato na kuiunganisha kompyuta hiyo na simu kwa njia ya *Bluetooth*.

Aliisoma taarifa ile, mara hii kwa utulivu. Mara kadhaa akimtupia jicho baba yake aliyekuwa akiangalia televisheni. Dakika chache baadaye aliinua simu na kuandika ujumbe kupitia

WhatsApp: *Duh, hizi nondo umezipata wapi?* Akatuma. Aliitazama simu hiyo ikituma ujumbe ule na kisha ishara kuwa ujumbe umefika ikajionesha. Sekunde chache zilikatika akiwa ameikodolea macho simu ikimwashiria kuwa Julius alikuwa akiandika kumjibu. Mara shah! Ujumbe kutoka kwa Julius ukaingia: *Siyo kitu kipya. Ukisoma ripoti mbalimbali ikiwemo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali vitu hivi vimetajwa. Yawezekana kuna uzembe au kukosekana kwa utashi wa kuchunguza na kuchukua hatua. Nimewatafunia. Kazi kwao kumeza.*

*Natamani ningekuwapo kwenye mkutano wako hiyo kesho*. Noela alihitimisha kwa ujumbe wa WhatsApp.

Licha ya hofu aliyokuwa nayo juu ya tuhuma hizi na nguvu ya kiutendaji waliyokuwa nayo watu hawa, alikuwa mwenye shauku ya kujua nini hatma ya jambo hili. Aliifunga kompyuta yake na taratibu aliinuka kuelekea chumbani.

*

Julius Mabala, akiwa nyumbani kwake Kinondoni Morocco Dar es Salaam, usiku wa manane, usingizi ulikuwa umepaa. Kichwani mwake yalipita mambo mengi yaliyohusiana na mkutano wake na waandishi wa habari hadi pale alipohisi uwepo wa mtu dirishani kwake akijaribu kuchungulia. Ndani kulikuwa kiza, hivyo mwangaza wa nje ulimwezesha kuona nje kupitia upenyo pale mapazia yanapokutana.

Taratibu aliliweka shuka pembeni na kwa hadhari kubwa akateremka kitandani na kunyata hadi dirishani. Kwa kutumia kidole alilisogeza pazia polepole na kupata fursa ya kutazama nje. Kwa sekunde kadhaa hakuona kitu kisha akamwona mtu aliyevaa kofia ya kininja, na nguo

nyeusi; bastola mkononi akinyata kuelekea upande mwingine wa nyumba. Mapigo ya moyo yalienda mbio, kijasho chembamba kikamtoka.

Kilitanda kimya kwa sekunde kadhaa na kisha ilisikika chekecheke ya funguo zilizoingia katika kitasa cha mlango ikifuatiwa na sauti za bawaba za mlango uliokuwa ukifunguka. Julius alipigwa na butwaa asijue la kufanya. *Amewezaje kufungua?* aliwaza. Hakuwa na silaha yoyote ya kuweza kukabiliana na mvamizi huyo. Aliyazungusha macho yake kwa haraka mle chumbani. Hakukuwa na sehemu ya kujificha. Wazo la kuingia uvunguni mwa kitanda alililitupilia mbali. Angekuwa amemrahisishia kazi mvamizi. Kujificha maliwatoni nako kungemaanisha kusalimu amri kirahisi. Mara macho yake yakaganda kwenye kabati na mara akakumbuka jambo. Wakati huo aliweza kuusikia unyayo wa mtu sebuleni. Alizama kabatini upesi na kimyakimya kama kivuli. Akabonyeza kitufe juu kulia na mlango wa siri ukafunguka. Akazama ndani zaidi; mlango wa siri ukajifunga. Nukta hiyohiyo ulisikika mshindo mdogo pale mlango wa chumba ulipovunjwa.

Julius alitulia tuli kusikiliza. Hakuwahi kuwaza umuhimu wa maficho haya ya siri hapo kabla. Kulikuwa na ukimya kisha akasikia mwaliko sauti wa swichi ya taa ya chumbani. Alishikwa na tumbo la kuhara. Kama tayari yupo chumbani atabaini kuwa kulikuwa na mtu chumbani humo kwani ufunguo ulikuwa nyuma ya mlango, simu yake ilikuwa kitandani, na hata mashuka kitandani yakiwa yamevurugwa kwa kulaliwa.

Kiza totoro kilitawala maficho hayo ya siri yaliyokuwa na upana mdogo tu kiasi cha kuweza kuhifadhi watu wawili hadi watatu. Sekunde

zikakatika. Mara kwa mbali akahisi uwepo wa mtu upande wa pili wa kabati. Miguu ilikuwa ikitetemeka, taratibu akashuka kwa lengo la kujikunyata mikono yote ikiwa imegusa kuta za maficho hayo. Mkono wake wa kushoto uligusa kitufe cha ukubwa wa kizibo cha soda na mara ghafla kilisikika king'ora kutoka katika fleti hiyo. Japo alikuwa ndani ya hifadhi hii ya siri, sauti hiyo kali ya king'ora ilimfanya mikono yote iende masikioni. Muda mfupi baadaye king'ora kikazima.

Ulitanda ukimya wa takribani dakika tatu kisha akasikia sauti zikipazwa kuliita jina lake. Alizitambua sauti zile za majirani zake na kutoka mafichoni.

"Kitu gani kimetokea?" alihoji mmoja wa majirani.

Akawasimulia mkasa mzima.

Dakika kadhaa baadaye, majirani walirejea katika fleti zao wakimwacha na maswali mengi yasiyo na majibu: *mtu huyu ni nani? Je alikuwa peke yake? Nia yake ilikuwa nini?* Mvamizi huyo hakuwa ameondoka na kitu. Simu, kompyuta na vitu vyote vya thamani vilikuwapo. *Huyu hakuwa kibaka, vinginevyo vyote hivi visingekuwapo.*

Zilikuwa zimesalia saa chache tu afanye mkutano wake na waandishi wa habari kuanika dili za kifisadi alizozichunguza akiwa mwanaharakati huru. *Je mvamizi huyu alikuwa na uhusiano na kadhia hiyo ya kifisadi? Je walikuwa wameamua kuisaka roho yake na kumnyamazisha? Yawezekana!* Alililikumbuka angalizo la mke wake kuhusiana na harakati hizi. Pengine harakati hizi zilikuwa zimeanza kuzaa visasi na sasa risasi zilikuwa zikiisaka roho yake.

Aliichukua simu yake na kumpigia dereva teksi aliyemfahamu afike hapo kumchukua. Dakika kumi

na tano baadaye alikuwa ameshafika. Alitoka upesi na kuufunga mlango wa nyumba.

Wakati wanaondoka alitazama nyuma kuhakiki kama kulikuwa na gari au pikipiki iliyokuwa ikiwafuata. Haikuwapo. Alikuwa hajaamua nini cha kufanya usiku huo. Jambo la muhimu ilikuwa ni kuondoka nyumbani kwanza kwani tayari palikuwa ni eneo hatarishi. Angeweza kukesha katika mojawapo ya klabu za usiku lakini alihitaji kupumzika. Alihitaji kupata usingizi mwororo kwani siku yote, tangu mawio hadi machweo alikuwa ameitumia kupitia nyaraka mbalimbali kujiandaa na mkutano wake na waandishi wa habari

Teksi ilimshusha Mlimani City. Alivuka eneo la maegesho ya magari hadi mlango wa klabu. Aliusukuma mlango mzito wa kioo na kutokea eneo la kukatia tiketi na walinzi. Alichukua tiketi yake kisha mmoja kati ya walinzi wawili wenye kushabihiana kwa urefu uliozidi futi sita na nusu, na mjengo wa miili iliyojaa misuli alimkagua kwa kutumia kifaa maalumu cha kielektroniki na kumruhusu. Aliusukuma mlango mwingine mzito na mara alikutana na alichokitarajia: muziki mzito, watu kibao wachangamfu wakicheza kwa raha zao—wengi wao wakitiwa hamasa na nguvu ya kilevi; wengine wakipaza sauti zao ziweze kusikika katika mdundo huo mzito ambao ungeweza kusababisha nyufa katika kuta za klabu hiyo. Julius alijipenyeza miongoni mwao, wengine wakimpiga vikumbo katika kucheza kwao, hadi ilipo kaunta ya baa na kuketi katika kiti kirefu cha kaunta, akaagiza mvinyo. Hakuwa anatumia kilevi lakini usiku huu alishawishika kuchangamsha akili.

Aligida mvinyo ule taratibu huku macho yake

yakivinjari ukumbi wa klabu. Watu walikuwa wenye furaha wakila bata huku yeye akitafakari madhila yaliyokuwa yakimkabili usiku huo na pia mkutano wake na waandishi wa habari. Ndani ya dakika kumi tayari alikuwa anashusha glasi ya tatu. Alikuwa akishindana na nafsi yake. Je ampigie simu mkewe kumjulisha juu ya tukio hilo usiku huo? Au akaushe hadi asubuhi? Hakuona sababu ya kukausha. Alikuwa amekata shauri na kuitoa simu yake mfukoni; akabofya mara kadhaa hadi ilipotokea namba ya mkewe, akabofya na kuiweka sikioni. Wakati akisubiri simu hiyo iite aligeuka na kuegama kwenye ubao wa kaunta, akiipa kisogo na kuutazama tena ukumbi wa klabu. Mara alikuwa kama aliyepigwa shoti ya umeme. Moyo wake ulipoteza mapigo kadhaa pale macho yake yalipotua kwa mtu aliyekuwa kavaafulana nyeusi ya mikono mirefu, suruali nyeusi na kofia akiingia klabu. Ubongo wake haukumdanganya. Mtu huyu alikuwa ni yuleyule aliyeingia nyumbani kwake. Kilichokosekana usoni mwake ni ile kofia ya kininja na bastola mkononi. Kwa haraka mno, ile taswira ya mtu yule na umbile lake vikamjaa akilini na ndipo mwili wake ukasisimka. Akaingiwa kiwewe asichokitarajia katika matendo yake. Hapo ndipo simu ya mkononi ilimponyoka, ikadondoka sakafuni na kusambaratika—betri huko, mfuniko kule. Aliteremka kitini macho yake yakiwa yameganda mwelekeo wa mtu yule japo alimpoteza kwa kukingwa na walabata. Aliyapepesa macho yake kutazama mahali simu yake ilijitawanya viungo vyake. Kilichofuata ni kuinama na kuokota injini ya simu, akalichukua betri kisha mfuniko na kuviswinda mfukoni bila kurudishia betri wala mfuniko. Hakurudi tena kuketi juu ya kiti kile

kirefu. Alichomoka kama mshale kuelekea msalani lakini badala ya kuingia mlango wa msalani alijipenyeza na kutokeza upande mwingine kulipokuwa na mlango wa kutokea. Alitembea haraka kadiri miguu yake ilivyomwezesha, akipumua kwa nguvu huku vitone vya jasho vikiwa vimejaa usoni kwake. Alipofika nje alipanda teksi ya kwanza iliyojitokeza mbele yake. Alikuwa amekata shauri kwenda kwa rafiki yake aitwaye Kiiza.

"Tunakwenda wapi?" aliuliza dereva teksi baada ya Julius kuingia ndani ya teksi na tayari akiwa kafunga mkanda.

"Sinza Mori."

"Kuna heri lakini? Naona kama…." aliuliza dereva teksi.

"Hakuna shari, ila nawahi jambo muhimu-endesha twende," aliamuru Julius.

Aliteremka mbele ya nyumba aliyokuwa akiishi Kiiza dakika kumi baadaye. Dereva teksi alimsubiri kuhakikisha kuwa Julius anafunguliwa mlango ndipo aondoke. Alibonyeza kengele ikaita. Wakati huo ndipo lilipomjia wazo kuwa angeweza kumpigia simu. Aliutumbukiza mkono mfukoni kutoa simu. Mkono ulipogusa betri akakumbuka kuwa simu ile ilikuwa imetawanyika vipande vipande. Wakati anatafakari ndipo mlango ulifunguliwa na Kiiza alisimama mbele yake.

"Kulikoni usiku wote huu?"

"Ni stori ndefu kaka," alijibu akipiga hatua kuingia. Kiiza alisogea pembeni kumpisha.

*

Shabi alikuwa na kasi na kila alichokifanya kilikuwa kwa usahihi kabisa na kama makosa yangekuwepo basi kiduchu bila kuathiri matokeo yaliyokusudiwa, lakini usiku huo mambo yalikuwa tofauti. Kama

siyo kile king'ora angekuwa amekwisha kutekeleza maelekezo yote aliyokuwa amepewa: "Tunamtaka akiwa hai, na ikiwezekana huo ushahidi anaodai kuwa anao tuupate." Hilo ndilo lilikuwa jukumu alilokuwa amepewa usiku huo—kuhakikisha anamteka Julius Mabala na kumfikisha kwa waliomwagiza.

Alikuwa amefanya kila kitu kwa usahihi: kuruka uzio, kujiridhisha kuwa Julius alikuwapo ndani, kufungua mlango kwa funguo bandia na kuingia hadi chumbani kwa Julius, lakini kabla hajamtia mikononi king'ora kikakatiza azma yake na kumlazimisha kuruka uzio na kurejea alikotoka.

Hakwenda mbali. Alirejea katika gari lililokuwa likimsubiri mtaa wa pili toka eneo la tukio, akiikunja ile kofia ya kininja na kuwa ya kawaida tu ikifunika nywele zake na ile bastola akiiswinda chini ya kitovu na kisha kuifunika na fulana. Alifungua mlango upande wa abiria na kuketi. Dereva, aliyekuwa pia mshirika wake katika operesheni ile alikuwa ameketi nyuma ya usukani.

"Vipi mbona umerudi fasta, umemkosa?"

"Sijui nimebugi wapi?" Shabi alijibu akiwa katika hali ya kukereka na masikitiko kwa wakati mmoja. Alikuwa ni mtu wa kupatia siku zote, "Nimemwona kwa macho yangu kupitia dirishani lakini nilipoingia ndani sikumwona na kabla sijaanza kumsaka king'ora kikalia. Sikuwa na jinsi ila kutimka."

Mlio wa king'ora ulikuwa umekata na ukimya ulikuwa umerejea katika eneo hilo. "Tuondoke," Shabi alimwambia dereva.

Taratibu dereva aliliondoa gari. Kulikuwa na magari mengine yakipita barabarani, hivyo uwepo wao eneo hilo pengine usingeweza kutiliwa shaka

yoyote.

Shabi alichomoa simu yake na kubonyeza programu maalum iliyomwezesha kumfuatilia Julius Mabala kupitia simu yake. Ilikuwa ni programu hii iliyokuwa imemwezesha kumpata Julius na kuwaongoza hadi nyumbani kwake na ilikuwa na uwezo wa kufuatilia simu husika hata kama imezimwa.

Akiwa bado anaitazama programu ile ilionesha kuwa Julius alikuwa katika mwendo. Alitazama katika hali ya utulivu kisha ramani katika programu hiyo ilimwonesha kuwa Julius alikuwa Mlimani City. Hawakuchelewa, nao wakaelekea huko.

Alipoingia ndani ya klabu, sehemu aliyokuwa na uhakika wa kumpata Julius aliangaza macho huku na kule. Kwa tukio lililotokea muda mfupi uliopita hakutarajia kumkuta miongoni mwa waliokuwa wakiserebuka na kupaza sauti. Aliitazama simu yake. Taarifa aliyoipata hapo ilimfanya aangalie eneo la kaunta na kufanikiwa kumwona akiwa katika mojawapo ya viti virefu vya kaunta, simu sikioni. Aliyarudisha macho yake upande mwingine wa klabu ambako nako kulikuwa na kaunta ya baa. Aliiendea kaunta ile na kuagiza bia ya Serengeti. Alipiga funda moja kubwa na kisha kugeuza uso wake kuangalia ile kaunta nyingine. Kwa mshangao Julius hakuwapo pale. Aliigeukia programu katika simu yake lakini haikuonesha kitu. Aliinuka upesi na kuelekea upande ule. Alipofika pale alipokuwa ameketi Julius; aliambulia kukuta nusu glasi ya mvinyo. Hakukuwa na dalili ya Julius kuwepo tena. Aliamua kwenda kumwangalia msalani. Hakuwepo. Programu katika simu yake haikuonesha kitu bado. *Huyu mwanaharamu imekuwaje?* aliwaza. Namna pekee ya kuzuia

programu ile isifanye kazi ilikuwa kuzima simu na kuondoa betri. Yawezekana ameng'amua hili? Mpango 'A' ulikuwa ni kumpata akiwa hai na kile alichodai kuwa ni vielelezo vitakavyowasilishwa mbele ya waandishi wa habari na iwapo ingeshindikana mpango 'B' ulikuwa ni kumshindilia risasi ya kichwa. Muda ulikuwa ukiyoyoma na njia pekee ya kufuata ilikuwa ni ile iliyohusisha mpango 'B'—risasi moja au mbili kichwani; lakini hata hili nalo lilionekana kuwa gumu kwani mlengwa alikuwa ameyeyuka kama moshi mawinguni.

Hadi alfajiri walikuwa ndani ya gari eneo la maegesho ya magari karibu na klabu moja ya usiku maeneo ya Kinondoni. Uchovu ulikuwa umewatawala, kuisisimua miili yao sigara ziliteketea midomoni mwao ikiwa ni bandika bandua. Na pengine kama wangekuwa katika mitaa ya uswahilini wangeishia kugonga sigara bwege. Hatimaye simu ya Shabi iliita. Aliitazama na kuipokea mara moja; akasikiliza kwa nukta chache kisha akajibu kwa kifupi: "Hatujafanikiwa…"

"Kuna mtu nakuunganisha naye atakuelekeza cha kufanya," ilisema sauti upande wa pili, "Nampa namba yako atakupigia muda si mrefu toka sasa."

Simu ikakatwa. Shabi aliingiwa na shauku kutaka kufahamu mtu huyo alikuwa na maelekezo gani kwake lakini kabla ubongo wake haujaendelea kuchakata taarifa ile; simu yake ikaita.

*

Siku moja kabla Nesto Balaga alikuwa katika shinikizo kubwa. Asubuhi hiyo ndiyo alikuwa amerejea nchini akitokea Brussels akiwa ni mmoja kati ya wajumbe wa ngazi za juu walioiwakilisha serikali katika mkutano wa Umoja wa Ulaya.

Walipokuwa tu wametua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ujumbe toka kwa Ben Samiku uliingia katika simu yake: *Tuonane Masaki mara ufikapo.*

*Nipe saa moja nitakuwa hapo.* Alijibu na kutuma

Walipotoka uwanja wa ndege alimwelekeza dereva ampeleke Masaki ambako Ben Samiku alikuwa akimiliki makazi ya kifahari. Iliwachukua takribani dakika hamsini hadi Masaki. Gari lao lilipokuwa mbele ya lango la kuingilia katika makazi haya ya Ben Samiku lango lilifunguliwa na mlinzi kijana aliyekuwa amevalia sare za bluu. Gari lao liliingia na kupaki katika maegesho ya magari ambapo kulikuwapo na mengine mawili—V8 na Benz. Jumba hilo la ghorofa mbili lilikuwa tulivu na nadhifu.

Ben Samiku alikuwapo mlangoni kumlaki, "Hongera bwana, mwenzangu umetoka kufaidi vya wazungu. *By the way Brussels* wanasemaje?"

"Huko kwema, tunamshukuru Mungu tumerejea salama."

Urafiki wao ulikuwa umedumu takribani miongo mitatu—tangu wakisoma chuo kikuu na baadaye katika utumishi. Siku hii hakukuwa na zile bashasha zilizozoeleka wakutanapo. Yaonesha kulikuwa na kitu kilichokuwa kinakwenda mrama. Walikwenda kuketi katika baa ndogo iliyokuwa na aina kadha wa kadha za vinywaji. Ben alimpatia kinywaji alichokipenda kisha wakiwa wote na vinywaji vyao mkononi alienda moja kwa moja kwenye mada husika: "Waikumbuka ile dili ya bilioni 330?"

"Naikumbuka."

"Kuna mtu anashupaza shingo yake. Amepanga kuitisha mkutano na waandishi wa habari kesho kuanika kadhia hii. Hii haipaswi kutokea."

Alifungua bahasha ya khaki na kutoa picha na kuziweka mbele ya Nesto.
"Naamini rafiki yetu Bozi atashughulikia hili."

Nesto aliitazama picha ile iliyokuwa imewekwa mbele yake. Ilikuwa ni picha ya kijana ambaye mara kadhaa alikuwa amewahi kumuona katika televisheni, hasa iliyohusisha mijadala mbalimbali ya kijamii, "Yawezakuwa kuna mtu aliye nyuma yake. Yawezekana anatumiwa na mahasimu wako."

"Uwezekano huo upo japo hadi sasa sijaweza kumhusisha yeyote na kijana huyu." Aliinua glasi yake na kupiga mafunda mawili kwa upesi, "*One step at a time.* Tumshughulikie yeye na iwapo kuna yeyote atajitokeza ni kufyekelea mbali."

*

Nesto Balaga alikuwa pia ni swahiba mkubwa wa Bozi Makamari. Uswahiba huo ulijengwa katika misingi ya nipe nikupe.

Bozi alikuwa anamiliki jengo la ghorofa tano lililoko mkabala na Mlimani City barabara ya Sam Nujoma. Ndani ya jengo hili ndimo zilimo ofisi za kampuni yake za ukandarasi na ile ya kuagiza na kusafirisha bidhaa nchi za nje—BozMax Contractors na BozMax Import & Export. Ofisi za kampuni zake hizi zilitwaa safu ya ghorofa yote ya tano huku safu za ghorofa zilizosalia zikiwa zimepangishwa kwa makampuni na mashirika mbalimbali.

Bozi Makamari alikuwa na umri wa miaka arobaini na nane, mrefu wa wastani, mpana kiasi mwenye kupenda kunyoa nywele zake na kubakia na upara na ndevu siku zote. Akiwa na umri wa miaka thelathini tayari alikuwa amesajili kampuni ya ukandarasi ya BozMax. Mwanzoni alipata kandarasi ndogondogo hadi neema ilipomwangukia pale alipoingia 'ubia' na watendaji

waandamizi serikalini. Nguvu yake iliongezeka siku hata siku kiasi cha kuweza kushinikiza na shinikizo likazaa matunda.

Bozi alizaliwa na kupewa jina Boaz. Baba yake aliyeitwa Mkama alikuwa karani wa mahakama ya mwanzo Nyanguge wilayani Magu, akisifika kwa kula mlungula ili kuwasaidia watu katika kesi zao. Fedha hizo za mlungula zilimfanya awe na utitili wa vimada na kusababisha fedheha ya kuitelekeza familia yake.

Siku moja Boaz akiwa na umri wa miaka kumi na mbili, arobaini za baba yake zilitimia pale alipokamatwa na kushtakiwa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa. Kesi iliunguruma kwa miezi miwili; ushahidi uliotolewa ulithibitisha pasipo shaka kuwa alikuwa na hatia ya kupokea rushwa. Alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu gerezani.

Katika hali ya kujaribu kuyamudu maisha ya familia mama yake alijiingiza katika utengenezaji na uuzaji wa pombe haramu ya gongo, Boaz akiwa ni sehemu ya mchakato mzima wa utengenezaji na uuzaji wa pombe hiyo haramu. Gongo alilolionja na kulikubali yeye lilikubalika kwa walevi wote. Boaz aliyekuwa mtoro shuleni aliacha kabisa. Akaanza kucheza kamari na watoro wenzie waliokuwa wakijishughulisha na uvuvi na vibarua vya hapa na pale.

Jioni moja Boaz alirejea nyumbani, akakuta pamepooza kama vile kuna msiba usio na waombolezaji. Palikuwa pamezoeleka kwa mishemishe za hapa na pale, walevi wakija kuburudika, wenye fedha na wasio na fedha, wenye kununua na wenye kudandia ofa.

“Mama yuko wapi?” Boaz alimuuliza mama wa jirani.

“Amekamatwa na polisi.”

“Polisi? Kwa kosa gani?”

“Kwani hujui gongo anayouza hapo nyumbani ni haramu?”

Haikuwahi kumwingia akilini kuwa gongo iliyokuwa ikiuzwa nyumbani kwao ilikuwa haramu.

Siku ya kesi mama yake alikiri kosa kwa kudhani kuwa mahakama ingemwonea huruma na kumwachia huru. Badala yake alihukumiwa kifungo cha miezi sita. Kuanzia hapo maisha ya Boaz yalichukua mkondo mwingine. Akawa mpweke. Muda wake katika vilinge vya kamari ukaongezeka.

Juma moja baadaye alipokea taarifa ya kifo cha mama yake baada ya kutokea mlipuko wa kipindupindu gerezani. Machozi hayakumtoka kwani alikuwa amelia mno kipindi chote tangu kukamatwa na kufungwa jela kwa mama yake. Kwa vile kipindupindu kilikuwa ndicho chanzo cha kifo hakuruhusiwa kwenda kumzika.

Asubuhi moja aliamua kuondoka nyumbani. Kituo cha kwanza kilikuwa mjini Mwanza; akipanga kwenda kwa mjomba wake. Mji ulikuwa mkubwa. Hakufahamu mtaa aliokuwa akiishi na hata aliowaulizia walibaki kumshangaa. Mawazo yake yalikuwa kwamba angempata kwa kuuliza lakini Mwanza ulikuwa mji mkubwa na siyo kama kijiji alichotoka. Hatimaye akajikuta miongoni mwa watoto wa mtaani.

Mtaani hapakuwa rahisi. Boaz alikuwa kama bundi aliyevamia kundi la mbayuwayu; kila mwenye ubavu alitaka apime ubavu wake kwake. Hata wale wadogo, chokambaya wakataka wamwonee. Hofu, woga na ugeni vilimfanya

akubali kuonewa katika siku za mwanzoni lakini baada ya kuzoea akawadhibiti mmoja baada ya mwingine. Hatimaye heshima ikachukua mkondo wake. Akajenga uswahiba na watoto wenzake na kupata wafuasi ambao waliungana kuepuka kuonewa na wenzao.

Kama walivyo watoto wengi wa mtaani alijifunza tabia ya kuchomoa na kukaba. Pesa iliyopatikana iliishia kwenye kamari. Akageuza kamari kuwa kila kitu kwake: njia ya kujikimu, starehe, burudani—akilala akiamka anawaza kamari tu. Taratibu jina lake likabadilika badala ya kuitwa Boaz Mkama likawa Bozi Makamari. Akalikubali jina hilo na kuanzia kipindi hicho ndilo jina alilojitambulisha nalo.

Ilipojitokeza fursa ya kupata mafunzo ya mgambo, akiwa na umri wa miaka kumi na nane, Bozi aliitumia fursa hiyo. Hamu yake kubwa ilikuwa ni kujifunza kutumia bunduki. Mwisho wa mafunzo Bozi alikuwa miongoni mwa wahitimu waliofanya vizuri hasa katika kulenga shabaha.

Miezi kadhaa baaadaye, akishirikiana na wenzake wawili, walifanikiwa kuwapora wafanyabiashara wa dhahabu waliokuwa wamewasili mjini Mwanza wakitokea Kahama ili kuuza dhahabu yao. Waligawana dhahabu ile; kila mmoja akashika njia yake na hawakuwahi kuonana tena. Bozi aliuza mgao wake wa dhahabu humo humo mjini Mwanza kisha akahamia Dar es Salaam ambako alijiingiza katika biashara ya kuuza magari. Miaka ikapita. Hakuwahi kufahamu alipoelekea baba yake baada ya kutumikia kifungo chake jela. Na hata alipofanya jitihada za kumtafuta haikufahamika aliko. Hatimaye akaanzisha kampuni ya ujenzi na baadaye ile ya kuagiza bidhaa

nje ya nchi. Ilikuwa ni katika harakati hizi ndipo alipoweza kujenga uswahiba na Nesto Balaga.

Bozi na Nesto walifahamiana miaka mingi iliyopita. Wakati huo Bozi alikuwa akifukuzia zabuni katika mojawapo ya idara za serikali. Aliimezea mate zabuni ile kwani alikuwa amejifunza kupitia kwa watu wake wa karibu kuwa 'serikalini kuna pesa—zabuni moja au mbili tu unaupa kisogo umasikini.' Hakujua ni mtu gani mwenye ushawishi ambaye angetia mkono wake pale.

Ilikuwa lazima apate pa kuanzia; Siku hiyo Bozi alifika katika ofisi iliyotangaza zabuni na kukaribishwa na mmoja kati ya makatibu wahtasi aitwaye Nasra.

"Nilikuwa na kitu muhimu ambacho nilitaka unisaidie," Bozi alimweleza katibu muhtasi, "Vipi unaweza kupata muda hata wakati wa chakula cha mchana tukala huku tunaongea?"

"*Yes*!" ilikuwa ni fursa nyingine adhimu kualikwa chakula cha mchana.

Mchana huo walikula chakula pamoja na maongezi yaliendelea wakati wa chakula. "Kuna ile zabuni iliyotangazwa ofisini kwenu, naitaka! Nimwone nani?"

"Zabuni ipi?"

"Ile ya ku-supply vifaa vya ofisi."

Hiyo mbona rahisi. Ukisema na Nesto, kila kitu umepata. Yeye ndiye mambo yote!"

Baada ya chakula Bozi alichomoa pochi yake iliyoshiba na kuhesabu noti kadhaa akaziweka mezani mbele ya Nasra.

"Hizi za nini?"

"Hiyo ni asante yangu kwa kukubali kuja," alitulia kidogo, "Nahitaji unisaidie jambo moja."

“Jambo gani?”

“Niandalie miadi na Nesto.”

“Nitaongea na katibu wake. Mara nyingi Nesto huwa yupo ofisini utamkuta tu.”

“*No*, sitaki miadi ya ofisini. Nataka iwe sehemu kama hii, ambapo tutaweza kuongea kwa uhuru zaidi.”

Uso wa Nasra ulijawa na mashaka, “Nesto ni bosi wetu; nawezaje kumleta huku?”

“Wewe si umesema nikitaka zabuni wa kumwona ni Nesto?”

“Ndiyo!”

“Basi tumia mbinu zote unazozifahamu! Mgao wako upo.”

Nasra alikuwa kimya, lakini ubongo ukitafuta jibu maridhawa.

“Jioni una ratiba gani?” aliuliza Bozi akiwa amemkazia macho, “Umeolewa? Una mume?”

“Mume sina ila nina boyfriend.”

Nikikualika kwa kinywaji jioni ya leo upo tayari?”

“Nipo tayari,” Nasra alijibu bila kupepesa macho.

Jioni siku hiyo Nasra alikuwa amejikwatua ile mbaya. Manukato yaliyoufunika mwili wakeyalikuwa ya gharama kubwa na yalitosha kuwa kilevi kwa Bozi. Walichukuana na safari hii Bozi alimchukua Nasra na kumpeleka katika hoteli ya kifahari iliyoko ufukweni mwa bahari ya Hindi.

Haikuishia hapo. Wakiwa wamelewa bwi, waliumalizia usiku wao pamoja katika chumba cha hoteli na kushuhudia mtanange wa wa mahabaya kukata na shoka.Jioni, siku iliyofuata, Bozi alipata fursa aliyokuwa akiiota; fursa ya kuonana na Nesto. Wakaongea ‘biashara.’

“Unajua pale yapo mabilioni ya shilingi?”

alisema Nesto.

"*Yes*!"

"Za kwangu ngapi?"

"Wewe taja tu kiasi," alisema Bozi kwa kujiamini.

Wakakubaliana mambo yote ya msingi. Urafiki wao ukaanzia hapo baada ya makubaliano. Na ule mchakato wa zabuni ulipokamilika majuma matatu baadaye kampuni inayomilikiwa na Bozi ndiyo ilikuwa imeshinda zabuni hiyo.

*

Taarifa kutoka kwa Nesto kwamba kuna mtu anataka kuchafua hali ya hewa ilitibua utulivu wote aliokuwa nao Bozi. Alitambua kuwa suala hilo lilihitaji kushughulikiwa mara moja. Suala hili lilikuwa sawa na maradhi ambayo yasipotibiwa mapema husababisha kilio kifo. Na hii haikuwa mara ya kwanza kushughulika na suala la namna hiyo

Nusu saa ilikuwa imepita tangu kupokea simu ya Nesto. Dereva aliyetarajiwa kufikishaujumbe aliwasili na kuruhusiwa kuonana naye moja kwa moja na kumkabidhi bahasha.

"Asante, nimeipata."

Ilikuwa ni kauli ya kumwondoa yule dereva. Akaondoka.

Bozi aliichana bahasha ile na kutoa picha. Aliitazama picha ile, *huyu ndiye anataka kuleta sekeseke?* aliwaza huku akiigeuza nyuma picha hiyo na kuyasoma maandishi mafupi yaliyoandikwa kwa mkono kwa kutumia kalamuya wino mwekundu,kabla ya kuirejesha picha hiyo katika bahasha na kisha kuitia kwenye droo ya meza alitafakari kwa sekunde kadhaa.

Bila kupoteza muda aliinua simu yake, "Njoo ofisini," alitamka baada ya simu ile kupokewa

upande wa pili.

Shabi, mmoja kati ya vijana wake wa kazi, aliwasili dakika ishirini baadaye. Shabi alikuwa amebakiza siku chache kutimiza umri wa miaka thelathini, mrefu wa wastani, si mnene wala mwembamba. Nywele zake zilikuwa fupi lakini zenye kutunzwa vema, akiachia sharubu fupi zikiwa zimeungana na ndevu na kunyolewa katika mtindo wa 'O'.

"Kuna kazi imejitokeza," alitulia, akameza mate kulainisha koo, "Kuna mtu ameitisha mkutano na wanahabari kesho. Mkutano huu haupaswi kufanyika kwa gharama yoyote na mhusika anatakiwa kupotezwa," aliongea bila kuonesha hisia zozote. "Lakini kabla tunamtaka akiwa hai na hivyo vielelezo vyake na kama itashindikana basi kikubwa ni kumwondosha bila kujali ni kwa namna gani."

Kwa takribani dakika mbili kimya kilitawala. Shabi aliutumia muda huo kuitazama picha ile. Ilikuwa ni ya kijana aliyemkadiria kuwa na umri wa miaka isiyozidi thelathini. Nyuma ya picha hiyo kulikuwa na maelezo yapata mistari minne ikiwepo anwani ya makazi.

"Nimemwona, na nadhani namfahamu huyu Julius."

"Jitahidi kusitokee makosa. Ukimpata nijulishe ili nikuelekeze pa kumpeleka."

Dakika tano baadaye Shabi aliiacha ofisi hiyo kichwani tayari akiwa na jina la mtu ambaye angeweza kumsaidia kazi hiyo.